**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI**

# MUHTASARI WA MAFUNZO YA UALIMU NGAZI YA CHETI ELIMU YA MSINGI

## TEHAMA

**2009**

© Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, 2009

ISBN: ………………………………………….

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuigwa, kunakiliwa, kutafsiriwa, kupigwa chapa au kutolewa kwa namna yoyote ile muhtasari huu bila idhini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Muhtasari huu umebuniwa na umetayarishwa na:
Taasisi ya Elimu Tanzania,
S.L.P. 35094,
Dar-es-Salaam
**TANZANIA**

Simu. + 255 22 2773005,
Faksi: + 255 22 2774420
Barua pepe: director.tie@tie.go.tz
Tovuti: www.tie.go.tz

## IDHINI

Mafunzo ya Ualimu wa Elimu ya Msingi Ngazi ya Cheti ni ya miaka miwili na yamekusudiwa kuandaa walimu mahiri wenye uwezo wa kufanya kazi kwa dhati. Walimu hao watafundisha katika shule za msingi. Mwalimu mwanafunzi atatambuliwa kuwa ni mwalimu baada ya kuhudhuria na kufaulu mafunzo ya cheti ya miaka miwili ambamo pia atafanya na kufaulu mazoezi ya kufundisha.

Andiko hili linaidhinishwa kuwa ni **Muhtasari wa Tekinolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) Mafunzo ya Ualimu wa Elimu ya Msingi Ngazi ya Cheti** wa mwaka 2009.

**Umeidhinishwa na ......................................................**

**Saini..................................................................................**

**Tarehe...................................................................2009**

**Kamishna wa Elimu**
Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi
S.L.P 9121
**Dar-es-Salaam**

Simu: +255 222 110150, 110179, 11046
Nukushi: +255 222 113271
Wovuti: www.moe.go.tz

## YALIYOMO

**Ukurasa**

Utangulizi………………………………………………………………………. iii

Madhumuni ya Somo la TEHAMA.......................................................................... iii

Malengo ya Mafunzo ya Ualimu ngazi ya cheti....................................................... v

Ujuzi katika Somo la TEHAMA…………………………………………………… v

Malengo ya Ufundishaji wa Somo la TEHAMA.................................................... vi

Muundo wa Muhtasari wa Somo la TEHAMA……………………………………. vi

Muda wa Mafunzo……………………………………………………………… vii

Upimaji wa Kozi........................................................................................................ vii

**MADA**

1.0 Misingi ya Ufundishaji na Ujifunzaji Somo la TEHAMA................................. 1

2.0 Maandalizi ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa Somo la TEHAMA...................... 2

3.0 Ufundishaji wa Mada za mufano..... .................................................................. 4

4.0 Upimaji.............................................................................................................. 13

Rejea ....................................................................................................................... 15

## UTANGULIZI

### Maelezo kuhusu Muhtasari wa Somo la TEHAMA.

Mafunzo ya Ualimu ngazi ya Cheti yamehusisha kozi ya ufundishaji na ujifunzaji wa somo la TEHAMA katika Shule za Msingi. Somo hili litasaidia kuandaa walimu wenye utaalamu wa kutosha katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la TEHAMA na hatimaye kukidhi malengo yaliyokusudiwa. Muhtasari huu umeandaliwa ili kukidhi haja ya ujifunzaji na ufundishaji wa somo la TEHEMA.

### Sababu za Kuwa na Muhutasari huu.

Kukua kwa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), kumeleta mabadiliko makubwa katika nyanja mbalimbali za maisha, kijamii, kiutamaduni, kielimu na kiuchumi, ambapo Teknolojia ya habari na mawasiliano imekuwa ni chachu ya maendeleo. Kwa kutambua umuhimu wa teknolojia hiyo, mwaka 2005 Tanzania ilianzisha somo la Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika mtaala wa elimu ya msingi. Ili kufanikisha ufundishaji na ujifunzaji wa somo la TEHAMA, wanahitajika walimu walioandaliwa vizuri katika kuutafsiri na kuutekeleza mtaala wa TEHAMA.

Somo hili litasaidia kuandaa waalimu wenye utaalamu wa kutosha katika ufundisahaji na ujifunzaji wa somo la TEHAMA kwa shule za msingi.

### Madhumuni ya Somo la TEHAMA

Mwishoni mwa mafunzo ya miaka miwili ya somo la TEHAMA, Mwanachuo aweze:

a) Kuwa mahili katika ufundishaji somo la TEHAMA katika shule za msingi.
b) Kutumia ujuzi wa TEHAMA katika kufundisha masomo mengine.

### Ujuzi katika Somo la TEHAMA.

Baada ya mafunzo ya miaka miwili (2), Mwanachuo anatarajiwa kuwa na ujuzi wa:-

a) Kutumia teknolojia na vielelezo katika ufundishaji na ujifunzaji.
b) Kuainisha mada za muhtasari wa TEHAMA na vitabu vya Kiada na Ziada kwa shule za msingi.
c) Kutumia azimio la kazi na andalio la somo katika ufundishaji na ujifunzaji somo la TEHAMA.
d) Kutumia misingi ya TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji.

e) Kuandaa mazoezi, majaribio na mitihani yenye kukidhi majazi yote ya kielimu.

**Malengo ya Ufundishaji wa Somo la TEHAMA**

Baada ya mafunzo ya miaka miwili (2), Mwanachuo aweze:-

a) Kujenga stadi za kubuni, kutengeneza na kutumia vielelezo vya kufundishia na kujifunzia somo la TEHAMA katika shule za msingi.
b) Kutambua mbinu za uchambuzi wa vifaa vya mtaala wa somo la TEHAMA kwa shule za msingi.
c) Kuandaa ufundishaji na ujifunzaji wa somo la TEHAMA.
d) Kutumia misingi ya ufundishaji na ujifunzaji wa somo la TEHAMA
e) Kutumia TEHAMA kukuza ufundishaji na ujifunzaji wa masomo ya sayansi, hisabati na lugha.
f) Kupima maudhui kwa kutumia jedwali la utahini.
g) Kutumia TEHAMA kukuza maarifa na stadi katika kushughulikia masuala mtambuko.

**Muundo wa Muhtasari huu wa Somo la TEHAMA.**

Muhtasari huu una sehemu kuu mbili, sehemu ya kwanza yenye kurasa za awali na sehemu ya pili yenye maudhui ya ufundishaji wa somo la TEHAMA. Sehemu ya kurasa za awali inajumuisha utangulizi, maelezo kuhusu mhutasari wa somo, sababu za muhtasari, ujuzi, malengo na madhumuni ya ufundishaji, mpangilio na uchaguzi wa mada na upimaji wa somo.

Sehemu ya pili inajumuisha maudhui ya ufundishaji wa somo la TEHAMA. Mada katika sehemu hii ni misingi ya ufundishaji na ujifunzaji, maandalizi ya ufundishaji na ujifunzaji, upimaji na mada teule. Mkufunzi anashauriwa kutumia njia shirikishi katika kuwezesha mada zote zilizo kwenye muhtasari huu.

Mada za somo hili zimechaguliwa kwa kuzingatia umuhimu wake katika kuwapa wanachuo stadi za msingi. Mada zimepangwa kwa mtiririko wa kimantiki, kuanzia misingi ya ufundishaji na kuelekea kwenye ufahamu wa kufundisha mada zilizoainishwa kwenye muhtasari. Mada mbalimbali zinazosaidia kujenga ujuzi fulani zimewekwa pamoja ili kujenga uhusiano. Mada kuu zote zina mada ndogo, ambazo ndizo zimejengewa malengo mahsusi na kupendekezewa

muda wa kuzifundisha. Aidha Muhtasari huu umebainisha mbinu, zana/vifaa na zana za upimaji mbalimbali ambazo mkufunzi atazitumia ili kumwezesha mwanachuo kuwa mahiri katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la TEHEMA. Mbinu, zana/vifaa na zana za upimaji zilizopendekezwa zimeainishwa kwa kuzingatia mazingira halisi ya vyuo na upatikanaji wa zana za kufundishia na kujifunzia. Mkufunzi anashauriwa kutumia mbinu na vifaa vilivyopendekezwa katika muhutasari huu.

Hata hivyo mapendekezo ya mbinu, zana/vifaa na zana za upimaji vinaweza kubadilishwa kulingana na mazingira ya chuo husika, lakini kigezo cha ubadilishaji wa mapendekezo kilenge kujenga mbinu shirikishi.

Mwisho wa muhtasari zimeorodheshwa rejea mbalimbali zilizotumika katika kuandaa muhtasari huu.

**Muda wa Mafunzo**

Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa somo la TEHAMA kwa shule za msingi litasomwa kwa miaka miwili. Shabaha ya somo hili ni kumwezesha mwanachuo kuwa na stadi na maarifa ya kufundisha somo la TEHAMA katika shule za msingi Tanzania.
Mwanachuo anatarajiwa kutumia masaa 128 katika muda wa miaka miwili kusoma somo hili.
Mafunzo kwa vitendo yatafanyika kwa wiki 16 katika miaka miwili.

**Upimaji na Tathimini**

Njia mbalimbali zitatumika kupima mafanikio na maendeleo ya mwanachuo. Njia hizo ni pamoja na majaribio, vitendo, kazi binafsi, mitihani ya muhula na mtihani wa kitaifa.

Mtihani wa kitaifa utatolewa na Baraza la Mitihani la Taifa ukiwa na jumla ya alama 25%. Alama za Upimaji endelezi zitaunganishwa na sehemu ya matokeo ya mtihani wa kitaifa.

Mafunzo kwa vitendo yatakuwa na upimaji wa pekee vivyo na tathmini yake.

Mapendekezo ya idadi, alama na njia za upimaji edelezi ni kama inavyooneshwa kwenye jedwali lifuatalo:-

| Na | Aina ya Upimaji | Idadi | Asilimia (%) |
|---|---|---|---|
| 1. | Majaribio | 3 | 5 |
| 2. | Vitendo | 2 | 5 |
| 3. | Kazi binafsi | 2 | 5 |
| 4. | Mitihani ya Muhula | 3 | 10 |
| | **Jumla** | | **25** |

## 1.0 MISINGI YA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA SOMO LA TEHAMA

**Muda: Masaa 8**

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii mwanachuo aweze:-

a) Kufafanua misingi ya ufundishaji na ujifunzaji wa somo la TEHAMA.
b) Kueleza umuhimu wa misingi ya kufundishia na kujifunzia TEHAMA.
c) Kutumia misingi ya ufundishaji na ujifunzaji wa somo la TEHAMA katika ujifunzaji na ufundishaji wa somo hilo kwa shule za msingi.

**Mbinu za kufundishia na kujifunzia Somo la TEHAMA**

a) Bungua bongo
b) Maktaba kutafuta nukuu za misingi ya ufundishaji na ujifunzaji wa somo la TEHAMA.
c) Majadiliano ya vikundi na uwasilishaji
d) Onesho mbinu katika vikundi na uwasilishaji juu ya namna ya kutumia misingi ya somo la TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji.

**Zana/Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia.**

a) Kompyuta iliyounganishwa kwenye intaneti.
b) Projekta
c) Manila
d) Bango kitita
e) Bango.
f) Kalamu za rangi
g) Muhtasari wa somo la TEHAMA shule za msingi
h) Rejea mbalimbali

**Upimaji.**

a) Mazoezi.
b) Utungaji wa insha.
c) Majaribio.
d) Kazi za vikundi

## 2.0 MAANDALIZI YA UFUNDISHAJI NA UJIFUNZAJI WA SOMO LA TEHAMA

### 2.1 Uchambuzi wa Muhtasari.

**Muda: Masaa 10**

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kupitia sehemu za awali za muhutasari.
b) Kutambua mada zilizomo katika muhtasari wa TEHAMA.
c) Kuoanisha mada zilizopo katika muhtasari wa TEHAMA na zilizopo katika vitabu vya Kiada na kiongozi cha mwalimu.
d) Kuainisha mpangilio wa mada katika muhtasari wa TEHAMA
e) Kuchambua mbinu za kufundishia na kujifunzia kwa kila mada katika muhtasari wa TEHAMA.
f) Kuchambua malengo mahsusi katika muhtasari wa TEHAMA
g) Kuchambua upimaji wa malengo mahsusi katika muhtasari wa TEHAMA.
h) Kuoanisha ujuzi na mada katika muhtasari wa TEHAMA.

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Maswali na majibu.
b) Majadiliano katika vikundi kuoanisha mada zilizopo katika muhtasari wa TEHAMA na zilizopo katika vitabu vya Kiada na Viongozi vya Mwalimu.
c) Majadiliano.
d) Matembezi ya galari katika kuchambua malengo mahsusi na upimaji wa malengo mahsusi katika muhtasari wa TEHAMA.
e) Ramani ya dhana katika kuoanisha ujuzi na mada katika muhtasari wa TEHAMA.

**Zana/Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia.**

a) Muhtasari wa TEHAMA kwa shule za msingi.
b) Kiongozi cha Mwalimu kwa shule za msingi somo la TEHAMA.

c) Vitabu vya Kiada na Ziada
d) Rejea mbalimbali.
e) Bango kitita
f) Gundi
g) Kalamu za rangi
h) Karatasi za manila.

**Upimaji.**

a) Mazoezi.
b) Majaribio katika kutaja mada na malengo mahsusi katika muhtasari wa TEHAMA.
c) Upimaji rika(peer assessment) juu ya taarifa za awali za maandiko mbalimbali ya mtalaa.
d) Upimaji wa pamoja kivikundi (Group assignment).
e) Mkoba wa kazi

**2.5 Kubuni na Kufaragua Zana.**
**Muda: Masaa 12**

**Malengo Mahsusi**

Baada ya Kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kueleza mbinu atakazotumia kuendeleza ubunifu wa zana za TEHAMA.
b) Kubuni zana za kufundishia na kujifunza Somo la TEHAMA
c) Kutengeneza zana za kufundishia na kujifunzia Somo la TEHAMA
d) Kukusanya vifaa vya kufundishia na kujifunzia Somo la TEHAMA
e) Kutumia zana katika ufundishaji na ujifunzaji wa Somo la TEHAMA

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Majadiliano.
b) Kazi mradi katika ubunifu wa zana za kufundishia na kujifunzia somo la TEHAMA

c) Onesho mbinu katika kufaragua zana za kufundishia na kujifunzia somo la TEHAMA.
d) Kazi Mradi katika kufaragua za za kufundishia na kujifunzia somo la TEHAMA.

**Zana/Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

a) Muhtasari wa TEHAMA kwa shule za msingi.
b) Makunzi halisi na yasiyo halisi
c) Vifani
d) Vifaa maalmu vya kutengenezea zana za ufundishaji.
e) Rejea mbalimbali.

**Upimaji**

a) Uchunguzi.
b) Mazoezi na majaribio.
c) Maonyesho ya zana za TEHAMA zilizotengenezwa na kufaraguliwa

## 3.0 Ufundishaji wa Masomo ya Mfano

### 3.1 Usikivu

**Muda: Masaa 10**

**Malengo mahsusi**

Baada ya Kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:

a) Kubaini mbinu mbalimbali za kufundishia mada ya usikivu.
b) Kuandaa zana na vifaa vya kufundishia mada ya usikivu.
c) Kuandaa somo juu ya mada ya usikivu.
d) Kufundisha somo la usikivu katika shule ya mazoezi
e) Kuendesha utafiti sanifu (action reseach)wakati wa somo la usikivu.

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Onesho mbinu.
b) Igizo dhima
c) Maswali na majibu.

d) Ufundishaji kiduchu

**Zana/Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

a) Redio
b) Maandiko
c) Luninga
d) Simu ya mezani au mkononi
e) Rejea mbalimbali.
f) Mhutasari wa TEHAMA wa shule za msingi

**Upimaji**

a) Uchunguzi wa kuona na orodha hakiki.
b) Mazoezi.
c) Fomu ya uchunguzi katika ufundishaji.
d) Mkoba wa kazi

### 3.2 Kueleza kwa Usahihi Habari Iliyosemwa

**Muda: Saa 8**

**Malengo Mahsusi**

Baada ya Kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:

a) Kubaini mbinu mbalimbali za kufundishia mada ya Kueleza kwa Usahihi Habari Iliyosemwa.
b) Kuandaa zana na vifaa vya kufundisha mada ya Kueleza kwa Usahihi Habari Iliyosemwa.
c) Kuandaa somo juu ya mada ya Kueleza kwa Usahihi Habari Iliyosemwa.
d) Kufundisha somo la Kueleza kwa Usahihi Habari Iliyosemwa.

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Maswali na majibu.
b) Bungua bongo.
c) Kazi mradi katika kusikiliza na kueleza habari iliyosemwa.
d) Ufundishaji kiduchu

**Zana/Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

a) Maandiko Mbalimbali
b) Redio
c) Luninga
d) Simu ya mkononi

**Upimaji**

a) Mazoezi mbalimbali ya kusikiliza na kueleza habari iliyosemwa.
b) Fomu ya uchunguzi katika ufundishaji kiduchu.
c) Mkoba wa kazi

### 3.3 Mawasiliano Kwa njia ya Alama

**Muda: Masaa 8**

**Malengo mahsusi**

Baada ya Kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze kumfundisha mwanafunzi:-

a) Kubaini mbinu mbalimbali za kufundishia mada ya Mawasiliano Kwa njia ya Alama
b) Kuandaa zana na vifaa vya kufundisha mada ya Mawasiliano Kwa njia ya Alama
c) Kuandaa somo juu ya mada ya Mawasiliano Kwa njia ya Alama.
d) Kufundisha somo la Mawasiliano Kwa njia ya Alama.

**Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji**

a) Kualika mgeni.
b) Ziara za Kimafunzo kuona alama na matumizi yake katika mawasiliano.
c) Majadiliano kivikundi na uwasilishaji.
d) Onesho mbinu kuchora alama sahihi za mawasiliano.
e) Ufundishaji kiduchu

**Zana/Vifaa vya kufundishia na Kujifunzia**

a) Bango kitita
b) Kalamu za rangi
c) Kitabu cha alama za barabarani
d) Moduli ya Usalama Barabarani
e) Alama mbalimbali za mawasiliano
f) Alama za wasioona.
g) Rejea mbalimbali

**Upimaji**

a) Maswali na majibu.
b) Majaribio na uwasilishaji.
c) Uchunguzi wa kuona na orodha hakiki.
d) Fomu ya uchunguzi katika ufundishaji kiduchu.

## 3.4 Alama za Kuashiria Hatari

**Muda: Masaa 8**

**Malengo Mahsusi**

Baada ya Kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:

a) Kubaini mbinu mbalimbali za kufundishia mada ya Alama za Kuashiria Hatari
b) Kuandaa zana na vifaa vya kufundisha mada ya Alama za Kuashiria Hatari
c) Kuandaa somo juu ya mada ya Alama za Kuashiria Hatari
d) Kufundisha somo la Alama za Kuashiria Hatari

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Kualika mgeni.
b) Majadiliano katika vikundi na uwasilishaji.
c) Kazi mradi katika kuchora alama mbalimbali zinazoashiria hatari.
b) Ufundishaji kiduchu

**Zana/Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

a) Picha na michoro ya alama zinazoashiria hatari

b) Bango kitita

c) Kalamu za rangi

**Upimaji**

a) Mazoezi.

b) Uchunguzi wa kuona na orodha hakiki.

c) Kazi mradi katika kubainisha alama mbalimbali zinazoashiria habari.

d) Fomu ya uchunguzi katika ufundishaji kiduchu.

## 3.5 Matumizi ya Maktaba.

**Muda: Masaa 8**

**Malengo Mahsusi**

Baada ya Kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:

a) Kubaini mbinu mbalimbali za kufundishia mada ya Matumizi ya Maktaba**.**

b) Kuandaa zana na vifaa vya kufundisha mada ya Matumizi ya Maktaba

c) Kuandaa somo juu ya mada ya Matumizi ya Maktaba

d) Kufundisha somo la Matumizi ya Maktaba

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Utatuzi wa tatizo.

b) Majadiliano kivikundi na uwasilishaji.

c) Maswali na majibu.

d) Onyesho mbinu katika kufundisha somo la matumizi ya makitaba.

e) Ziara mafunzo katika maktaba.

f) Kazi mradi katika kutafuta maandiko mbalimbali katika maktaba.

g) Ufundishaji kiduchu.

**Vifaa/ Zana za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Maktaba halisi

b) Chumba cha maktaba

c) Vitabu

d) Kadi za Katalogi

e) Bango kitita

f) Kalamu za rangi
g) Rejea mbalimbali

**Upimaji**

a) Mazoezi na majaribio.
b) Uchunguzi makini na orodha hakiki.
c) Fomu ya uchunguzi katika ufundishaji kiduchu.

## 3.6 Matumizi ya Vituo vya Habari na Mawasiliano

**Muda Masaa 8**

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:

a) Kubaini mbinu mbalimbali za kufundishia mada ya Matumizi ya Vituo vya Habari na Mawasiliano
b) Kuandaa zana na vifaa vya kufundisha mada ya Matumizi ya Vituo vya Habari na Mawasiliano
c) Kuandaa somo juu ya mada ya Matumizi ya Vituo vya Habari na Mawasiliano
d) Kufundisha somo la Matumizi ya Vituo vya Habari na Mawasiliano

**Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji**

a) Fikiri, jozisha na shirikisha/wasilisha.
b) Bungua bongo, maswali na majibu.
a) Ziara mafunzo kutembelea vituo vya habari na mawasiliano.
b) Kualika mgeni kutoa mada ya umuhimu wa kituo cha habari na mawasiliano
c) Ufundishaji kiduchu.

**Vifaa/Zana za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Majarida
b) Vipeperushi
c) Redio
d) Luninga
e) Kompyuta iliyounganishwa na intaneti

f) Rejea mbalimbali.

**Upimaji**

a) Mazoezi na majaribio katika kueleza dhana ya vituo vya habari na mawasiliano na umuhimu wake.
b) Mkoba wa kazi
c) Fomu ya uchunguzi katika ufundishaji kiduchu.

## 3.7 Vituo vya Ushauri Nasaha

**Muda Masaa 8**

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze kumwezesha mwanafunzi:-

a) Kubaini mbinu mbalimbali za kufundishia mada yaVituo vya Ushauri Nasaha
b) Kuandaa zana na vifaa vya kufundisha mada ya Matumizi ya Vituo vya Ushauri Nasaha
c) Kuandaa somo juu ya mada ya Matumizi ya Vituo vya Ushauri Nasaha
d) Kufundisha somo la Matumizi ya Vituo vya Ushauri Nasaha

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Bungua bongo.
b) Majadiliano.
c) Manila
d) Karamu za rangi
e) Kualika mgeni kueleza dhana ya vituo vya ushauri Nasaha.
f) Ziara mafunzo kutembelea vituo vya ushauri nasaha.
g) Ufundishaji kiduchu.

**Zana/Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

a) Majarida
b) Vipeperushi
c) Redio
d) Luninga

e) Kompyuta iliyounganishwa na intaneti.

f) Rejea mbalimbali

**Upimaji**

a) Mazoezi na majaribio.

b) Mkoba wa Kazi.

## 3.8 Huduma ya Posta

**Muda: Saa 14**

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:

a) Kubaini mbinu mbalimbali za kufundishia mada ya Huduma ya Posta

b) Kuandaa zana na vifaa vya kufundisha mada ya Huduma ya Posta

c) Kuandaa somo juu ya mada ya Matumizi ya Huduma ya Posta

d) Kufundisha somo la mfsno (demonstration) Matumizi ya Huduma ya Posta

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Maswali na majibu.

b) Kualika mgeni.

c) Onesho mbinu juu ya uandishi sahihi wa barua, kutuma na kupokea barua, vifurushi, hawala ya fedha, rejista.

d) Ufundishaji kiduchu.

e) Ziara mafunzo kutembelea kituo cha posta.

**Vifaa/ Zana za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Bahasha

b) Stempu

c) Karatasi

d) Gundi

e) Kitabu cha orodha za anwani

f) Kifani cha Sanduku la Posta

g) Rejea mbalimbali

h) Bahasha ya rejista
i) Barua
j) Fedha
k) Rula
l) Kalamu
m) Fomu ya kutuma barua au fedha
n) Stakabadhi
o) Kadi ya kupokea rejista
p) Rejea mbalimbali
q) Mhutasari wa somo la TEHAMA shule za msingi

**3.9 Kutumia Mbinu/njia za Mawasiliano ya kisasa**

**Muda: Saa 10**

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:

e) Kubaini mbinu mbalimbali za kufundishia mada ya Kutumia Mbinu/njia za Mawasiliano ya kisasa
f) Kuandaa zana na vifaa vya kufundisha mada ya Kutumia Mbinu/njia za Mawasiliano ya kisasa.
g) Kuandaa somo juu ya mada ya Matumizi ya Kutumia Mbinu/njia za Mawasiliano ya kisasa
h) Kufundisha somo la mfsno (demonstration) Matumizi ya Kutumia Mbinu/njia za Mawasiliano ya kisasa.

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Maswali na majibu.
b) Kualika mgeni.
c) Onesho mbinu juu ya  matumizi ya fax, simu za mkononi, barua pepe.
d) Ufundishaji kiduchu.
e) Ziara mafunzo kutembelea vituo vya mawasiliano.

**Vifaa/ Zana za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Simu ya mkonono
b) Mashine ya faksi
c) Vivuli vya faksi
d) Rejea mbalimbali
e) Computer iliyounganishwa na internet
f) Mhutasari wa somo la TEHAMA shule za msingi

## 4.0 UPIMAJI

### 4.1 Mazoezi ya Darasani

**Muda: Masaa 8**

**Malengo mahsusi**

Baada ya Kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kuandaa mazoezi ya darasani
b) Kusahihisha mazoezi ya darasani.
c) Kuandaa maswali ya mbalimbali.

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Bungua bongo.
b) Majadiliano kivikundi.
c) Onesho mbinu.
d) Kazi binafsi kuandaa mazoezi ya darasani na mwongozo wa usahihishaji.
e) Kazi mradi katika kuandaa mazoezi, kusahihisha na kuandaa maswali mbalimbali.

**Zana/Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

a) Mutasari wa somo la TEHAMA kwa shule za msingi.
b) Nukuu mbalimbali zinazohusiana na somo la TEHAMA
c) Karatasi za kuandikia
d) Kalamu
e) Rejea mbalimbali

**Upimaji**

a) Mazoezi na majaribio katika kuandaa mazoezi ya madarasani.

b) Mkoba wa kazi kutunza mazoezi mbalimbali ya darasani.
c) Uchunguzi wa kuona orodha hakiki katika kuandaa mazoezi darasani na mwongozo wa usahihishaji.

**4.2 Majaribio na Mitihani**

**Muda: Masaa 8**

**Malengo mahsusi**

Baada ya Kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kuandaa jedwali la kutahini la mada za TEHAMA.
b) Kutunga maswali yanayokidhi mahitaji ya majazi na ngazi zake
c) Kusahihisha na kuweka alama za majaribio na mtihani.
d) Kutunza kumbukumbu za maswali ya majaribio na mtihani.

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Onyesho mbinu juu ya uandaaji wa jedwali la kutahini.
b) Majadiliano kivikundi.
c) Kazi binafsi katika kutunga maswali ya majaribio, mtihani na mwongozo wa usahihishaji.
d) Kazi mradi utungaji wa mtihani na mwongozo wa usahihishaji.

**Zana/Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

a) Mfano wa jedwali la utahini
b) Muhtasari wa somop la TEHAMA kwa shule za msingi
c) Nukuu mbalimbali zinazohusiana na TEHAMA
d) Karatasi za kuandikia
e) Kalamu
f) Rejea mbalimbali

**Upimaji**

a) Mazoezi na majaribio katika kuandaa jedwali la utahini, majaribio mitihani na mwongozo wa usahihishaji.
b) Mkoba wa kazi wa kutunza mitihani na majaribio.

**REJEA**

Taasisi ya Elimu Tanzania (2005); Mwongozo wa Kufundishia / Kujifunzia somo la TEHAMA katika Shule za Msingi

Wizara ya Elimu na Utamaduni (2005). Muhtasari wa TEHAMA kwa Shule za Msingi

Ministry of Education and Vocational Training (2007); Information and Computer Studies Pedagogy syllabus for Diploma in Secondary Education.

Tanzania Institute of Education (2005). Framework for the review of certificate teachers Education Curriculum.